# Mwongozo wa Jamii kwa Mpango Kazi wa Watu Maalum wa Mfuko wa Kimataifa 2014-2017

eannaso

Regional Platform
for Communication and Coordination
on HIV/AIDS, Tuberculosis and Malaria
For Anglophone Africa

# MPANGO KAZI MAALUM NI NINI?

Mpango Kazi Maalum wa Mfuko wa KImataifa (2014-2017) ni andiko ambalo linaelezea mipango ya kuimarisha kazi na athari za Mfuko wa Kimataifa kulingana na Watu Maalum (Key Population).

Hebu tuitizame hio kwa undani:

## (WATU MAALUM) (MPANGO KAZI)

**WATU MAALUM NI MAKUNDI YA WATU AMBAYO:**

1. Yanapata athari kubwa za magonjwa
2. Yanapata huduma hafifu
3. Yapo katika watu ambao wamezuiwa kisheria ama wametengwa

**MPANGO KAZI** ni dira/ mwongozo wa mchakato wa jinsi malengo yatafikiwa na athari zake

Kwa ujumla, Mpango unasisitiza malengo ya Mfuko wa Kimataifa katika kufikia mahitaji na haki za watu maalum. Mipango inalenga kuimarisha kazi na athari za Mfuko wa Kimataifa kulimgana na watu maalum. Mfuko wa Kimataifa unataka kulenga uwezo wake katika huduma ambazo zinaumuhimu zaidi na ambazo zina athari kubwa zaidi, na ina aminika kwamba hii inapatikana kwa watu maalum.





## ZAIDI KUHUSU WATU MAALUM

### *3,1 Watu maalum ni nani?*

Watu maalum katika mipango ya Ukimwi:

- Mashoga, watu ambao wanavutiwa wa mapenzi kwa jinsia zote (bisexual) na wanaume wengine wanaofanya mapenzi na wanaume wenzao
- Mtu yoyote anayejidunga sindano za dawa za kulevya
- Wauza ngono
- Watu waliobadilisha jinsia (transgender)

Watu Maalum katika mipango ya Kifua Kikuu:
- Wafungwa
- Watu wanaoishi na Ukimwi
- Wahamiaji
- Wakimbizi
- Watu wa asili

Watu Maalum katika mipango ya Malaria
- Wahamiaji
- Wakimbizi
- Watu waliofurushwa makwao
- Watu wa asili katika maeneo yaliathirika na malaria

Pia, watu wote waishio na Ukimwi na ambao wana Kifua KIkuu ama wamepona, wako katika maelezo haya ya Watu Maalum.

## KWANINI TUNAHITAJI KUWALENGA HAWA WATU MAALUM?

Watu maalum ni muhimu katika kushughulikia Ukimwi, Kifua Kikuu na Malaria kwa njia muafaka. Mfuko wa Kimataifa unaamini kwamba watu maalum wanatoa maoni muhimu (mitazamo, mwongozo na tathmini) kutokana na uzoefu wao wa moja kwa moja na juhudi zao binafsi katika kushughulikia magonjwa haya matatu. Kutokana na hili, Mfuko wa Kimataifa unataka Kujenga uhusiano nao pamoja na kufanya nao kazi.

Karibia watu milioni 9 wanapata maambukizi ya Kifua Kikuu kila mwaka na asilimia 95% ya kesi hizi zinatokea katika nchi zinazoendelea.

Watu maalum wanakumbwa na kiwango kikubwa cha maambukizi kuliko watu wa kawaida

## SEHEMU KUU MBILI YA MPANGO KAZI

***Azma kuu mbili kuu za Watu Maalum***

- Mfumo mpya wa Ufadhili
- Mfumo mpya wa Uratibu wa Nchi (CCM) wa kuweza kupata pamoja na viwango

***Azma kuu mbili kuu za Mpango Kazi***

- Kujenga Uwezo
- Kuhamisha Jamii

## KWA NINI KUHAMASISHA JAMII?

- Watu maalum wanahitaji msaada kutoka kwa mifumo ya kijamii kuliko makundi mengine.
- Mitandao ya kijamii na mashirika ya msaasa, uenezi na udugu ni muhimu kwa watu maalum.
- Kuimarisha mitandao hii ya kijamii na mashirika inaweza kuwa na athari chanya kwa watu maalum
- Kukua kwa mitandao ya kitaifa, kikanda na kimataifa ambayo inawakilisha watu maalum ni muhimi sana
- Njia moja ya kupata msaada kwa mitandao hii ni kupitia kuimarisha ufadhili wa mifumo ya kijamii

## KUJENGA UWEZO

Mpango wa Kuimarisha Mifumo ya Kijamii (CSSF) inasisitiza umuhimu wa Kujenga uwezo kwajili ya mipango bora ambayo ni endelevu kwa jamii.

Mpango huu (CSSF) unatambua umuhimu wa mashirika ya kijamii na mitandao katika kutoa huduma, uenezi na kuwafikia watu katika jamii zilizoathirika. Hata hivyo, viwango vya ufadhili bado uko chini.

Mfuko wa Kimataifa unategemea kuimarisha athari za CSSF kupitia kuongeza uwekezaji na kupitia kukusanya taarifa kuhusu maendeleo ya shughuli za kuimarisha mifumo inayofadhiliwa inavyoendelea. Tarrifa hizi zinaweza kusaidia katika kufanya maamuzi ya ugawaji wa fedha za CSSF ilikuleta manufaa zaidi.

Uwekezaji katika CSSF inaweza kuongeza uwezo wa watu maalum kushiriki na kufuatilia Mifumo ya Uratibu wa Nchi pamoja na michakato mingine ya utawala wa Mfuko wa Kimataifa.

Nyongeza nyingine katika uwekezaji wa CSSF unaweza kuimarisha ushiriki wa matu maalum katika kuandaa maombi ya ufadhili na utekelezaji wa mipango. Kwa hili, bodi ya Mfuko wa Kimataifa umepitisha mpango maalum wa kutoa usaidizi wa kitaalam kusaidia Kujenga uwezo na ushiriki wa watu maalum na jamii katika mazungumzo ya nchi.

Mpango una malengo matano ili kuhakikisha watu maalum na mahitaji yao yanajumuishwa katika kila hatua ya utoaji wa ufadhili.




| MALENGO MADHUBUTI | HII INAMAANISHA NINI? |
|---|---|
| 1. Uwekezaji unaolenga watu maalum | 1. Kuongeza uwekezaji katika huduma na mipango kwajili ya watu maalum ambayo ni bora na inayofikia watu. |
| 2. Kujumuisha kwa watu maalum katika michakato ya nchi na kikanda | 2. Kupata sauti (mitazamo) ya watu maalum kwa kuhakikisha kwamba mashirika yanayosaidia yana rasilimali na nyenzo za kufanya kazi yao na kueneza ujume. |
| 3. Kuandaa malengo yanafikika na kuimarisha jinsi ya kuripoti. | 3. Kuimarisha upatikanaji na utumiaji wa ufadhili kuwa mashirika yanayoshughulikia watu maalum |
| 4. Kuimarisha ujuzi miongoni mwa wafanyakazi na washirika wa Mfuko wa Kimataifa | 4. Kuhakikisha wale wote wanaofanya kazi na watu maalum wanajua mengi kuhusu watu hao na wanahabarishana. |
| 5. Uongozi na uenezi kutoka kwa na pamoja na watu maalum | 5. Kuhakikisha wale wote wanaofanya kazi na watu maalum wanapata taarifa zote kuhusiana na mahitaji ya watu hawa na ujuzi huu unasambazwa ili Kujenga utamadumi mzuri. |

## WASILIANA NA MPANGO WA KIKANDA

Regional Platform for Communication and Coordination for Anglophone Africa Hosted by EANNASOArusha, TanzaniaTel: +255 737 210598Email: eannaso@eannaso.org | Website: www.eannaso.org
Facebook: www.facebook.com/eannaso.org | Twitter: @eannaso